**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Shule ya sekondari Mawenzi
S.L.P 478
MOSHI
JUNI 2021

Namba za simu
Simu ya shule 0737- 950170
Mkuu wa Shule 0767-74 09 08
Makamu Mkuu wa Shule 0755-31 01 37

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi…………………….
S.L.P…………………………………………….
…………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAWENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI MKOA KILIMANJARO MWAKA 2020**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2021 kwenye tahasusi ya ………… Shule ya Sekondari Mawenzi ipo umbali wa kilometa tatu Magharibi mwa mji wa Moshi. Usafiri wa basi kutoka mjini Moshi unapatikana katika kituo cha mabasi Moshi nauli ni shilingi 400/=.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe……………………Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………………..Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………………………

Shule yetu ipo barabara ya Arusha karibu sana na Uhuru Hotel na Redio Sauti ya Injili. Wanafunzi wanaotoka / wanaopitia barabara ya Arusha – Moshi washuke kituo cha **MEMORIAL** na maeneo mengine washukie kituo kikuu cha mabasi Moshi ni rahisi kuchukua tax hadi shuleni.
Kama umekubali nafasi hii tekeleza maagizo yaliyoorodheshwa na jaza fomu A, B na C na kuzirudisha shuleni siku utakapowasili.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare ya shule**

(a) Sketi mbili (2) ndefu hadi kwenye kiwiko cha mguu, (**tafadhali mzazi zingatia hili**) rangi ya kijivu, mshono rinda box.
(b) Mashati mawili meupe za mikono mirefu.
(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni suruali mbili za jezi rangi ya bluu.
(d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(e) Soksi fupi jozi mbili nyeupe za shule
(f) Sweta rangi ya kijivu yenye “V” shingoni.
(g) Sketi nyeusi mbili (2) ndefu za kufika kwenye kiwiko cha mguu zenye marinda ya kufuatana zitakazovaliwa siku za Jumamosi na Jumapili na baada ya masomo. Hutaruhusiwa kuvaa nguo nyingine kinyume na hizo. Huruhusiwi kuja na sweta, jacketi au koti la aina nyingine yoyote.
(h) Wanafunzi wa Kiislam wanaruhusiwa kuvaa juba (isiwe na urembo wowote) nyeupe tu wakati wote wakiwa shuleni. (zisipungu nne)
(i) T /Shirt 2 nyeupe zisizo na maandishi wala mchoro.(shingo iwe ya mduara)
(j) Raba za michezo rangi nyeupe
(k) Truck suit mbili rangi ya Dark Blue.

### 2.2 Ada na michango ya shule

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi shilingi 70,000/= Unaweza kulipa nusu 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

**Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :-**

*a)* Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
*b)* Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
*c)* Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
*d)* Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
*e)* Shilingi 3,000/= nembo ya shule
*f)* Shilingi 15,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs 10,000/= na Bima ya Afya Tshs 5,000/=
*g)* Shilingi 10,000/= kukodisha godoro kwa mhula.
*h)* Fedha ya tahadhari 5000/= (haitarejeshwa)

**JUMLA KUU NI TSH 174,000/=**

Fedha zote hapo juu zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **40301200137** kwa jina Mawenzi Sekondari katika Benki ya NMB ( **tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).**

**Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :-**

(a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
**(b)** Nakala ya result slip ya kidato cha nne
(c) Ream moja ya karatasi A4 (No 1).
(d) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ( orodha imeambatanishwa)
(e) Scientific calculator na Mathematical set (kwa tahasusi za HGE na EGM.
(f) Shuka mbili za rangi ya light blue.
(g) Bed cover moja nyeupe isiyo na urembo wa aina yoyote
(h) Chandarua nyeupe (mosquito net)
(i) Blanketi moja rangi yoyote.
(j) Nguo ya kulalia (nightdress)
(k) Kanga / kitenge jozi MOJA TU. Mitandio na vitambaa vya kichwa haviruhusiwi.
(l) Taulo, mswaki, malapa (umoja au bata) na rain boot, mwavuli na mafuta ya kupaka yasiyo na harufu kali
(m) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(n) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
(o) Sanduku MOJA la bati na begi dogo la kubebea vitabu vya darasani
(p) T shirt za kuvaa mwanafunzi akiwa nje ya shule itapatikana shuleni kwa sh. 15,000/= (sio lazima) (Ac No 42210006428)
(q) Bima ya Afya (NHIF) kulingana na maazimio ya kikao cha wazazi sh. 50,400/= kwa wasiokuwa na bima ya afya. Hii ni muhimu sana.(Ac No 42210006428)

TANBIHI: Mwanafunzi aje na barakoa na kitakasa mikono.

### 2.3 VIFAA VYA USAFI

| **S/N** | **HGK** | **HGL** | **HKL** | **EGM** | **HGE** |
|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Fagio la chelewa | Fagio la chelewa | Fagio la chelewa | Fagio la chelewa | Fagio la chelewa |
| **2.** | Water squizer | Sabuni ya maji lita 5 | Dawa ya choo lita 5 (disinfectant) | Soft broom | Panga lililonolewa |
| **3** | Sabuni ya maji lita 5 | Reki | Panga lililonolewa | Sabuni ya maji lita 5 | Dawa ya chooni lita 5 (disinfectant) |
| **4.** | Fyekeo lililonolewa | Fyekeo lililonolewa | Fyekeo lililonolewa | Fyekeo lililonolewa | Fyekeo lililonolewa |

## 2.4 VIFAA VYA MASOMO

I. Madaftari makubwa (counter books) nane (8) ya kuandikia notes (yanapatikana katika duka la shule)
II. Kalamu za kutosha, rula na penseli (vinapatikana duka la shule)
III. Picha passport size 4 za rangi ya bluu
IV. Wanafunzi waje na Oxford Advanced learners' dictionary pamoja na vitabu vya kiada anavyoweza kupata (Orodha imeambatanishwa).
V. Wanafunzi waje na vitabu vya ibada kwa mujibu wa madhehebu yao.

## 3. VIFAA AMBAVYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NAVYO:

Ni marufuku mwanafunzi kuwa na vifaa visivyoruhusiwa shuleni ikiwa ni pamoja na simu za mkononi, redio au redio cassette, pasi ya umeme, heater, kamera, vyakula vya aina yoyote, vileo vya aina yoyote, viatu nje ya sare ya shule, nguo binafsi (ambazo sio sare ya shule), hot pot, thermos, vidani n.k. Vifaa hivyo vitachukuliwa na havitarudishwa na mhusika ataadhibiwa.

## 4. SHERIA ZA SHULE

Sheria / kanuni / Taratibu za shule ni lazima zifuatwe na zimeambatanishwa na fomu hii ya kujiunga ( Joining Instruction).

## 5. MWISHO

Kwa niaba ya walimu na wafanyakazi wengine na Bodi ya Shule nakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii na ninakukaribisha katika shule yetu. Ni imani yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa.

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**Saini ya Mkuu wa Shule…………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: CHRISTINE ROGATH**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule……………………….**

## SHERIA ZA SHULE

Sheria zote za shule zimewekwa kwa walengwa /wanafunzi kulifikia lengo lao la kuwepo hapa shuleni.

1. Kuwa mwanafunzi unapaswa **KUJITAMBUA** kuwa wakati uwapo mwanafunzi wa shule ya Mawenzi Sekondari unaishi ndani ya utaratibu wa kiuwanafunzi ndani na nje ya shule, usiku na mchana.

2. Kuongeza muda wa **RUHUSA HALALI** mfano kwenda hospitali, posta, n.k. ni kosa litakalosababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali.

3. Mwanafunzi haruhusiwi kuchelewa kurudi shuleni wakati wa likizo. Anapochelewa afike shuleni siku na saa za kazi akiwa na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni. Fika na barua iliyopitishwa na **MRATIBU ELIMU KATA** anapotoka, la sivyo atarudishwa nyumbani. Muda wa mwisho kuripoti ni saa 10:00 jioni. Wanafunzi wa mbali wafike siku moja kabla.

4. Kutii viongozi ni wajibu wa kila mwanafunzi. Wanafunzi wawaheshimu na kuwatii **WALIMU WOTE NA WAFANYAKAZI WASIO WALIMU, WAGENI WOTE** wanaoitembelea shule, viongozi wote na Taifa na Umma na viongozi wanafunzi.

5. Mwanafunzi anatazamiwa kufanya kila kazi, iwapo ana matatizo ya kiafya mzazi/ mlezi atapaswa kutuma taarifa ya daktari kwa mkuu wa shule. Shule haitoi special diet kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ya chakula.

6. Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu au kupigiwa simu. Iwapo kuna jambo muhimu mzazi wasiliana kwa namba ya shule (0737 950 170) siku na muda wa kazi.

7. Wageni wa aina yoyote hawaruhusiwi kufika / kupita eneo la mabweni. Mwanafunzi harusiwi kuongea na mtu yeyote asiyekuwa mwanajumuiya wa shule hii katika eneo lolote la shule.

8. Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya eneo analohitajika kuwepo. Ni lazima awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule mfano kuitika mara moja na kukimbia na kuelekea mahali atakiwapo wakati anaposikia kengele au mwito mwingine, shughuli za uzalishaji mali, roll-call, usafi wa mazingira, michezo, kinyume na hapo ataadhibiwa vikali.

9. Ni maarufuku na kosa kubwa sana kwa mwanafunzi kuendesha au kushiriki katika vyama ambavyo havitambuliwi na uongozi wa shule. Haruhusiwi kuchezea vilabu vya michezo nje ya shule.

10. Nywele fupi zisizozidi urefu wa robo inchi na daima ziwe zimechanwa ndizo zitakazoruhusiwa. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kunyoa kipara,panki/kisahani au kuweka dawa ya aina yoyote. Adhabu itatolewa kwa yeyote atakayekiuka. **Hereni, mkufu, bangili, pete, vipini, kofia, shanga, miwani ya jua, rangi za kucha**, **hina, “lipstick”** na vitu vingine vitakavyomfanya mwanafunzi kutokuwa na mwonekano wa kiuanafunzi haviruhusiwi.

11. Ruhusa kutoka nje ya shule hutolewa na Mkuu wa Shule au na Mwalimu mwingine kwa idhini ya Mkuu wa Shule. Kibali kiwe na saini pamoja na mhuri wa shule. Kibali cha kuhudhuria msiba kitatolewa kwa mwanafunzi aliyefiwa na baba au mama, (wazazi halisi wa mwanafunzi) dada au kaka wa kuzaliwa tumbo moja. Hakuna ruhusa itakayotolewa kwa jamaa wengine zaidi ya hao.

12. Wakati mwanafunzi awapo nje ya shule kwa ruhusa ni lazima awe amevaa sare ya shule, pia anapokwenda likizo na wakati wa kurudi.

13. Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelea nyumba za watumishi bila sababu ya msingi. Kukiwa na dharura viongozi watahusika kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu au mkuu wa shule.

14. Mzazi au mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa itakapolazimu kufanya hivyo na si vinginevyo.

15. Haruhusiwi mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani mbali na sare iliyoelekezwa.

16. Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja kwa sababu zisizo za msingi wakikutwa wataadhibiwa vikali.

17. Hairuhusiwi mwanafunzi kuhama domu au chumba alichopangiwa adhabu kali itachukuliwa.

**1. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ulevi wa aina yoyote na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Kuanzisha, kuchochea au kushiriki mgomo au fujo shuleni.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule, walimu au watu wengine.
6. Kutoheshimu Bendera ya Taifa, alama au fedha ya Taifa.
7. Kupata au kutoa mimba ndani na nje ya shule.
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutohudhuria shuleni kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa
10. Kukataa adhabu ya Mkuu wa Shule.
11. Kupigana na mwalimu/,mfanyakazi au mwanafunzi.
12. Kukutwa na simu ya mkononi, *line, USB*, redio, CD n.k.
13. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
14. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika wa maaru fu kama “ Twende Kilioni”. Kuwepo na sababu MAALUMU ya kuruhusu mwanafunzi kusuka.
15. Kufuga ndevu
16. Kuvuta sigara
17. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
18. Kusababisha mimba au kumpa mimba mwanafunzi.
19. Kwenda kwenye nyumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
20. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
21. Kutoroka na kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule

**TANBIHI**

Tutakuwa na kikao cha wazazi wote wa kidato cha tano na sita tarehe **21/08/2021.** Tafadhali sana mzazi usipange kukosa kikao kikao hiki. Ni muhimu sana kwa maendeleo ya binti yako.

**FOMU A:**

**Kiambatisho I:**

PICHA YA MWANAFUNZI

**HATI YA MAKUBALIANO**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MAWENZI,
S.L.P 478,
MOSHI.

**<u>KUKUBALI NA KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE:</u>**

Mimi ……………………….……………nakubali nafasi ya kidato cha ……tahasusi ya …………niliyopewa katika shule yako.
Nayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wa shule na wafanyakazi kama walezi wangu.
Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

**JINA LA MWANAFUNZI:……………………**  **SAHIHI:…………………**

**JINA LA MZAZI /MLEZI:……………………………**  **SAHIHI:…………**

Anwani ya Mzazi /Mlezi:……………………………………………………………..
Namba ya simu…………………………………………………………………

Namba ya kuandikishwa:………………………Tarehe………………….
Darasa ulilopangwa:……………………………Bweni……………………

| | **SHULE ALIYOMALIZA KIDATO CHA NNE** | **NAMBA YA SHULE NA NAMBA MTIHANI** | **CHAGUO** | **ALAMA ULIZOPATA KATIKA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **HISTORY** | **GEOGRAPHY** | **KISWAHILI** | **ENGLISH** | **MATHS** |
| A | **JAMHURI** | **S.0328/04** | **HGK** | **C** | **D** | **B** | | |
| | | | | | | | | |

**FOMU B:**
**Kiambatisho II**

**SHULE YA SEKONDARI MAWENZI,**
**S.L.P 478,**
**MOSHI.**
**TAREHE:……………………………**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**JAZA FOMU HII KWA UKWELI HII NI SIRI KATI YAKO NA MKUU WA SHULE TU:**

1. Andika majina kamili.
   i. Majina ya Shule……………………………………………………………………………
   ii. Majina ya nyumbani…………………………………………………………………………..

| **MAJINA** | **La kwanza** | **La kati** | **La mwisho** | **UMRI** | **TAREHE YA KUZALIWA** |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANAFUNZI | | | | | |
| BABA /MLEZI | | | | | |
| MAMA/MLEZI | | | | | |

**2. NYUMBANI:**
Kijiji/Mtaa……………Kata…………………Tarafa……………….Wilaya………….Mkoa…………………

3. Anwani ya nyumbani…………………………………………Simu:……………………………………

4. Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa nani…………………………………………………..
Uhusiano na wewe?..........................................................................................................
Anafanya kazi gani na wapi…………………………………………………………………………

5. Wazazi na Ndugu:
Baba yuko hai?................................................Mama yuko hai?..................................
Baba ana watoto wangapi?.........................Wavulana……………Wasichana………………
Baba ana wake wangapi?............................wewe ni mtoto wake wa ngapi?...............
Mko wangapi kwa mama huyo? …………………wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama….
Dini yako……………………………..madhehebu………………………………………………………..

**UNAOWATEGEMEA:**

a) Unaishi na nani na wapi?...........................................simu yake……………………
b) Nani anayekupa mahitaji ya shule:……………………simu yake……………… SAHIHI:………………
   **TOA SABABU KAMA SIYO MZAZI**:………………………………………………………………
c) Wakati wa likizo utaenda wapi…………………………….uhusiano………………………anaishi wapi…………………………………………….namba ya simu……………………………………………………….

Majina ya watu 4 watakaohusika kuwasiliana na uongozi wa shule endapo utahitajika kwa suala lolote lile.

| | **JINA** | **ANWANI** | **SIMU** | **UHUSIANAO** | **MAHALI ANAPOISHI** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |

**PICHA ZA WATU WANAOHUSIKA KUWASILIANA NASHULE**

| BABA AU MLEZI<br>1 | MAMA AU MLEZI<br>2 | NDUGU<br>3 | NDUGU<br>4 |
|---|---|---|---|

**FORM C**

**MAWENZI SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 478**
**MOSHI.**

To be completed by a Medical Officer from a recognized Government Hospital NOT HEALTH CENTRES AND DISPENSARIES

Full Name of Student………………………………………………… sex/female……………………….
Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………………..
Stool examinations……………………………………………………………………………………………
Sexually Transmitted diseases…………………………………………………………………………
T.B.Test…………………………………………………………Skin………………………………………….
Eye Test………………………………………………………Ears……………………………………………..
Chest …………………………………………………………Spleen………………………………………….
Abdomen…………………………………………………….
U. P. T……………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION:**
E.g. Physical defects/impairment, pediatric disorders
……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………….

I certify that the above student is fit/unfit to pursue studies as stated above.

Signature:……………………………………………………………………………………………..
**MEDICAL OFFICER**

**DATE: ………………………………………………….. (Rubber Stamp) ………………………………..**

Note: Students should send or bring the completed form to school

**ORODHA YA VITABU**

1. **ADVANCED MATHEMATICS**
   a) Advanced Mathematics Form V, Vi By Gdy Publishers
   b) Understanding Pure Mathematics By Chandler.
   c) Advanced Level Pure Mathematics By C.J Tranter.
   d) Advanced Mathematics for secondary school – Septine I. Sillem.
   e) Pure Advanced Mathematics – J.K. Backhouse.

**2. BAM**
(1) Basic Applied Mathematics By Wakamoga Masinde
(2) Basic Applied Mathematics By Gdy Publication.

**3. Economics**
(1) Modern Economics By Hardwick $4^{th}$ Ed
(2) Simplified Economics. N. A. Salemi

**4. Kiswahili**
**1.** Kamusi ya Kiswahili sanifu (TUKI ) 2015
2. Kitangulizi cha tafsiri nadharia na mbinu- Mwansoko
(1) Massamba D.P ( ) Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu Tuki, Dar Es Salaam.
(2) Massamba D.P Na Wenzake ( ) Sarufi Miundo Ya Kiswahili Sanifu Tuki, Dar Es Salaam.

**Riwaaya**
(3) Shafi Adam (1999) Vuta Ni Kuvute Mkuki Na Nyota Publishers Ltd, Dar Es Salaam.

(4) Msokile . Mbunda (2007) Usiku Utakapokwisha Macmillan Aidan Lts Dar Es Salaam.
(5) Tuwa Hussein (2007) Mfadhili Macmillan Aidan Ltd Dar Es Salaam.
(6) Robert . S. ( ) Kufikirika. Oxford University Press Nairobi.

T**amthiliya**
(7) Hussein Ebrahim (1988) Kwenye Ukingo Wa Thim Oxford University Press
(8) Mohamed .S. (1990) Kivuli Kinaishi Oxford University Press Nairobi.
(9) Muhando P. (2007) Nguzo Mama Macmillan Aidan Ltd Dar Es Salaam.
(10) Mbogo Emmanuel ( 2007) Morani. Macmillan Aidan Ltd Dar Es Salaam.

**Ushairi**
(11) Mvungi T. (1985) Chungu Tamu T.P.H Dar Es Salaam
(12) Khatibu S. (2007) Fungate Ya Uhuru Macmillan Aidan Ltd Dar Es Salaam.

(13) Haji Gora ( 2001) Kimbuga Tuki Dar Es Salaam.
(14) Rober S. ( ) Mapenzi Bora Mkuki Na Nyota Publishers Dar Es Salaam.

**5. English**
(1) Oxford Advanced Learners Dictionary
(2) Advanced Level English: A Practical Aproach.Nicholaus Asheli,Good Book Publishers

(3) Literature For Advanced Level:Godfrey Ruta Bukagile.Nyambari Nyangwine Publishers
(4) English For A Level—Oxford
(5) Advanced level English Language 1 - Shadrack G. Ndambo and James Egino Kinunda
(6) Literature review for Advance Level – Shitundu
(7) Poetry analysis for A level and O level – Shitundu
(8) Introduction to literature - Shitundu

6. **History**

(1) Advanced Level History Paper One N. A. Paper Two. Kato Abubakar
(2) Essentials In Advanced History.

**7. Geography**

(1) Integrated Approach. D.T Msabila
(2) Physical Geography –RB. Bunnet
(3) Research Methodology By Kothan
(4) Landforms of Africa - Maxmillan

8. **General Studies**

(1) Understanding Advanced Level General Studies – Bigirwamungu J. & Deogratias S.
(2) Advanced Level General Studies Notes – Nyanwine, N.